BEST SELLER

# MILIKI KIWANDA MILIKI UCHUMI

## MILIKI KIWANDA NYUMBANI KWAKO




PIUS M. JUSTUS

# YALIYOMO

| | |
|---|---|
| Yaliyomo | i |
| Mawasiliano | ii |
| Hati miliki | v |
| Shukrani | vi |
| Utangulizi | vii |
| Dhana ya ujasiriamali | 1 |
| Mradi wa Chaki | 12 |
| Sabuni ya mche | 30 |
| Sabuni ya maji (1) | 38 |
| Sabuni ya maji (2) | 41 |
| Shower Jelly | 44 |
| Tiles Cleaner | 49 |
| Sabuni ya chooni | 51 |
| Hand sanitizer | 53 |
| Sabuni ya Unga | 55 |
| Batiki | 60 |
| Mishumaa | 63 |
| Shampoo | 65 |
| Lotion | 67 |
| Jam Fruit | 72 |
| Mafuta ya Mgando | 74 |

Tambi za dengu 76
Crisps/clips 78
Windows cleaner 80
Jik 81
Unga wa lishe 83
Tomato Saurce 85
Sabuni ya Mwarobaini 87
Sabuni ya Parachichi 89
Sabuni ya Carrot 91
Sabuni ya Papai 93
Lebo 95
Vifaa vya Usalama 97
Sehemu ya kupata Malighafi 98
Video za mafunzo 99
Jiunge na group yetu ya whatsapp 101

**MAWASILIANO**

**PIUS MULIRIYE JUSTUS**
**+255 754 745 798/+255 652 128 567**
**Whatsapp 0754745798 / 0659908078**

**piusjustus28@gmail.com**
**www.piusjustus.com**

**December 2016**

PJ PROJECTS
Suluhisho La Mjasiriamali.
0659908078 | 0754745798

## Jiunge na group yetu ya whatsapp



KITABU HIKI KIMEANDIKWA NA;

PIUS M. JUSTUS

SIMU: +255 754 745 798 / +255 659 908 078

BARUA PEPE: piusjustus28@gmail.com

FACEBOOK: PIUS JUSTUS MULIRIYE

INSTAGRAM: @piusjustusmuliriye

TWITTER: @MULIRIYEPIUS

WEBSITE: www.piusjustus.com

TOLEO LA KWANZA DECEMBER 2016.

Pius Justus Muliriye ni mjasiriamali, mwandishi, mhamasishaji na mnenaji ambae ameamua kufanya kazi hii ya kuhakikisha kua unapiga hatua katika kuinua kipato chako kila siku kupitia anachokiandika na kukinena. Karibu sana ukutane naye kwenye kitabu hiki cha  Kwanza cha."**Jinsi ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za ujasiriamali**"

Ni imani yangu kuwa maisha yako hayatakuwa kama yalivyokua baada ya kusoma kitabu hiki.

# HATI MILIKI

Haki zote za kitaaluma zimehifadhiwa haipendezi na ni kinyume na sheria kunakili au kuchukua chochote kilichoandikwa katika kitabu hiki bila idhini kutoka kwa mwandishi wa kitabu hiki; lakini kinaruhusiwa kutumiwa popote palipo na mafundisho yanayohusiana na yaliyoandikwa humu kwa ruhusa ya mwandishi.

Kwa matumizi ya kitabu hiki katika mafundisho tafadhali wasiliana na mwandishi kwa mawasiliano yaliyopo hapo juu.

## MAOMBI YANGU KWAKO

Kitabu hiki ni kwa ajili yako wewe tu uliyenunua, ni vyema kabisa ukamwelekeza anaehitaji aje kununua kuliko kumtumia nakala hii itamfanya yeye aone thamani ya kitu alichokilipia kama wewe. Tafadhari sana nakuomba ufanye hivyo ili uweze kuwasaidia wengine waweze kutambua ujuzi huu kwa gharama zao. Asante sana.

# SHUKRANI:

Wapo watu wengi sana wamehusika katika kuniwezesha mimi kufikia hapa nilipo hadi kutoa kitabu hiki. Wapo niliowapa kipaumbele cha kuwepo kwenye kitabu hiki kwa maana nisingeweza kuwaandika wote.

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu kwa Mungu mkuu muumba wa vyote na anaetupatia uwezo, akili na maarifa kwa ajili ya kuifanya dunia kua sehemu bora zaidi.

Baba na Mama yangu mzazi Justus Muliriye na Adelina Bissama, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wazazi wangu walionilea katika maadili mema na nikaweza kufika hapa nilipo. Wamenitunza na kunionyesha njia bora ambazo ninazitumia ili kufanikiwa. Wamenivumilia pale nilipokosea. Kitabu hiki kikawe furaha kwao kwa kutambua kua walizaa mtoto wa pekee sana duniani. Mungu awabariki na kuwaongezea maisha marefu duniani wafaidi matunda ya watoto wao.

Wadogo zangu Francis Yustus, Eva Yustus, Evodia Yustus, Sophia Yustus na Charles Yustus kwa kuniombea mimi kufanikisha hiki nilichokifanya


PJ PROJECTS
Suluhisho La Mjasiriamali.
0659908078 | 0754745798

# UTANGULIZI

Taaluma ya ujasiriamali nchini Tanzania Imeanza kushika kasi zaidi miaka ya 1990 baada ya mashirika yasiyo ya kiserikali kuieneza kwa wananchi na baada ya miaka michache pía serikali ilianzisha mikakati mbalimbali katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu ya ujasiriamali ili kuinua hali za maisha.

Elimu ya ujasiriamali ilianza kutolewa kwa nijia za useminishaji, warsha na makongamano kwa wafanyabiashara wadogowadogo kama wauza mbogamboga, nguo vyakula, vinywaji, na biashara zingine ndogondogo. Taaluma hii ilipokelewa kwa upotofu nchini Tanzania kutokana na kuonekana kuwalenga wafanyabiashara wenye hali za chini. Watu wengi waliiona haina faida kwao hata mitaala ya vyuo hapa nchini haikutilia maanani taaluma ya ujasiriamali.

# UTANGULIZI

Ujio wa utandawazi, sayansi na teknolojia na mabadiliko ya tabía ya nchi ni kati ya sababu zilizoamusha umma wa watanzania wasomi kwa wasiosoma, masikini kwa matajiri na kuiona taaluma ya ujasiriamali kwa jicho pembuzi na yakinifu kuwa ni zaidi ya wafanyablashara wadogo.

Hivi leo vijana wengi wasomi kwa wasiosoma wanabuni,kuanzisha na kuendesha vitega uchumi mbalimbali vikubwa kwa vidogo.Pia wengine wamediriki hata kukimbia kazi za kuajiriwa ili waingie kwenye ujasiriamali ambao umeonekana kuwa na mafanikio makubwa nchini Tanzania kutokana na nchi hii kujaa fursa mbalimbali za uwekezali mitaji zinazokuza biashara na uchumi kwa ujumla.

Kitabu hiki kinaibua na kuchokonoa hisia kali zenye kuleta mapinduzi ya kifikra juu ya dhana nzima ya ujasiriamalí kwa vijana na wazee bila kuangalia viwango vya mitaji yao, elimu na mazingira wanayoishi.

Katika kitabu hiki mjasiriamali anayeanza na anayeendelea atajifunza mambo mengi ikiwa pamoja na dhana ya ujasiriamali utafiti wa kijasiriamali,huduma za ukuzaji biashara,uendeshaji miradi,utunzaji wa kumbukumbu za biashara,mifano ya wajasíriamali nchini ,mipango kazi ya miradi huduma kwa wateja n.k.

Kitabu hiki cha Elimu ya Ujasiriamali ni cha pekee na cha aina yake nchini Tanzania.Kitabu hiki ni díra ya mafanikio kwa watafuta maendeleo kote nchini iwapo kitatumiwa vizuri na mtu, watu au taasisi fulani. Tafti mbalimbali zimefanyika juu ya maudhui mbalimbali yaliyomo katika kitabu hiki.

# SURA YA KWANZA
# DHANA YA UJASIRIAMALI
# (THE CONCEPT OF ENTREPRENEURSHIP)

Dhana ya ujasiriamali imeanza kuchipuka zaidi Kama taaluma inayojipambanua miaka ya 1940. Somo la ujasiriamali lilitambulishwa rasmi katika mitaala ya uchumi yachuo kikuu cha Harvard, taaluma hii hatimaye ilianza kuenea kote duniani.

Kufikia miaka ya 1980 baadhi ya nchi za kiafrika zilíkuwa zimeanza kujifunza somo la ujasiriamali kama nyenzo ya ukuzaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na vikundi. Hivi leo dhana ya ujasiriamali inazidi kupanuka kila siku ikihubiriwa na viongozi wa dini serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa miongozo ya kukuza uchumi.

Hivyo UJASIRIAMALI ni mchakato wa kuibua fikra za kibunifu na kuanzisha miradi yenye mbinu na mikakati mipya ya uzalishaji mali na uendeshaji.Ujasiriamali ni mawazo bunifu ya uendeshaji biashara kwa njía mpya zilizobuniwa kutokana na udhaifu uliopo katika zile za awali hali kadhalika ujasiriamali huja na ugunduzi wa mradi au mikakati katika mazingira yaliyopo.

**MJASIRIAMALI**

**(AN ENTREPRENEUR)**

Ni mtu yeyote anayebuni, kuanzisha na kuendeleza miradi kwanjia za pekee katika uzalishaji. Aidha mjasiriamali anaweza kuwa mtu yeyote anayetoa mwongozo wa kuendesha mradi kwa mtu au watu wengine.

Uchumi ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika jamii au nchi kwa ujumla.

Biashara ni ununuzi na uuzaji wa bidhaa au huduma fulaniyenyea lengo la kupata faida.

Ujasiriamali ni hali ya uwekezaji mtaji katika biashara bila hofu ya kupata hasara. Kwa kutumía fafanuzi hizo fupi ni dhahili kuwa ujasiriamali ni kitendo cha kuweka maarifa yenye kiwango cha juu zaidi katika biashara fulani au huduma na kuiendesha kwa njia za kibunifu kuimalisha uzalishaji wenya tija.

## SIFA BAINIFU ZA MJASIRIAMALI

(a) Kujitoa mhanga

Mjasiriamali lazima ajitoe mhanga kupambana na vikwazo, majanga na watu wenye lengo la kumkatisha tamaa. Pia ajitoe mhanga kuuweka mtaji wake bila hofu ya kupoteza na hata akipoteza aweke tena na tena na tena bila kukata tamaa (A risk taker).

(b) Mvumbuzi na mgunduzi (creative and innovative)

Schumpeter alisema,"....Ili mtu aitwe mjasiriamali anatakiwa kuvumbua au kungundua mradi ambao katika mazingira yake haupo au upo lakini autafutie maboresho yatakayoouonesha mradi wake kuwa ni wa kipekee katika uzalishaji bidhaa.

(c) Mvumilivu

Mjasiriamali inampasa kuwa mvumilivu katika mradi wake. Ajenge uvumilivu katika kusaka malighafi,masoko pia kupambana na matatizo katika mradi wake.

(d) Mtumiaji mzuri wa fursa

Fursa za kijasiriamali zipo nyingi sana kulingana na mazingira alipo mjasiriamali, hivyo mjasiriamali hana budi kuzitumia.

(e) Anatakiwa awe mtu wa kujituma

Kujituma kunaenda sambamba na uchapakazi (hardworking) ili kuleta mafanikio.

(f) Mtunza kumbukumbu

Mjasiriamali anayetunza kumbukumbu za mradi wake anaweza kupanga malengo mazurikwa kuangalia alikotoka.

(g) Kujiamini (self confidence)

Mjasiriamali anatakiwa kujisimamia katika fikra zake, malengo na hata kufanya maamuzi magumu bila hofu ya hasara au kusemwa vibaya na watu.

Je mjasiriamali huzaliwa au hutengenezwa? Ni hoja ambayo imekuwa ikisumbua watu wengi katika mijadala. Baadhi huamini kuwa mjasiriamali huzaliwa na kipaji cha kubuni,kuanzisha na kustawisha miradi.Hawa hutumia mifano ya watu waliofanikiwa kibiashara bila kufundishwa au makabila fulani yanayoendesha biashara tangu
zama za kale Wengine hutumia kigezo cha mazingira ambayo mjasiriamali huzaliwa,mazingira yanayompa fursa ya kujifunza mbinu za ubunifu na uendeshaji miradi.Ukweli ni kwamba mazingira anayoyakuta mjasiriamali huyu pamoja na vipaji vyake baada ya kuzaliwa ndiyo yatakayo muongoza katika kubuni ,kuanzisha na kuendeleza miradi.

Mjasiriamali wa kuzaliwa au kujifundishwa hana budi kujifunza juu ya uwepo wa fursa, uendeshaji,sera na kanurni za mazingira ya nchi husika.

**KUMBUKA**: Wajasiriamalí huifuata fursa badala ya fursa kuingojea ije. Wanaoifuta na kuivumbua hupata faida nyingi zaidi na wale ambao husubiri fursa ivumbuliwe ndipo waige huambulia faida kidogo na mara nyingi huwa ni hasara.

Hivyo utafiti wa kijasiriamali huanza na uhitaji,soko,chanzo cha bidhaa, unafuu wa manunuzi, ubora, uhalali na uhakika.Haya huweza kuifanya biashara au mradi wako kustawi vizuri.

## UTAFITI WA KIJASIRIAMALI

Zipo tafiti kadhaa katika taaluma ya kijasiriamali ambazo zimekuwa zikifanyika, zinafanyika na zitaendelea kufanyika kulingana na mabadiliko ya uzalishaji na ushindani wa kimasoko

(a) Utafiti wa mahitaji

Mjasiriamalia kabla hajaanza biashara, mradi au kutoa huduma aifikiriayo anatakiwa kutafiti.
Je jamii hiyo ina uhitaji wa biashara hiyo? Je wangapi wanatoa huduma kama hiyo na kwa mtindo gani? Je unazo mbinu za ushindani dhidi yao? Na utafiti wa uhitaji ni muhimu sana kabla ya kuanza hatua yeyote.

Damalisa (28) wa Namanyele Nkasi Mkoani Katavi kabla hajafungua mradi wake wa usindikaji viatu vya kina mama alitafiti na kuona kuwa wanawake wengi wa Namanyele hasa kina dada wanapenda viatu vilivyotengenezwa kwa njia za kiasili.

(b) Utafiti wa masoko

Soko la bidhaa au huduma sio lazima liwepo mahala ambapo mjasiriamali analshi.Mfano soko la asali ya Tabora linaweza kuwa nje ya mkoa huo.

Hivyo mjasiriamali kupitia utafiti wamasoko imara unaweza kumpatia ushindi mkubwa wa kukuza na kupanua mradi wake. Mbinu kadhaa za kujilmarisha katíka soko lako ulilolivumbua ni pamoja na;

(i) Bei yako iwe ya kati hata kama huna
mshindani kwani kitendo cha kupandisha ní kujikaribishia washindani.

(ii) Chunguza zaidi ubora wa bidhaa yako kabla ya kuiweka mbele ya mteja.

(iii) Lugha na kaulí nzuri kwa wateja
wako. Epuka lugha za maringona ulalamishi jitahidi kumjalí mteja wako tena íkiwezekana umbembeleze hata kama utafanya biashara yenye faida ndogo.Faida yako pale itakuwa kutangazwa vizuri kwa wengine kupítia mteja mmoja.

(iv) Usafi huanzla eneo la kutolea huduma

yako, usafi binafsi (mwili na mavazi), usafi wa bidhaa au huduma utoayo. Mfano, Maabara yako inatakiwa kuwa katika hali ya usafi kuanzia mtoa huduma, vyombo, viti na hata muonekano wa jengo uwe mzuri ili kumpa imaní na mvuto mteja wako.Halikadhalika kwa watoa huduma za vyakula na vinywaji.

(v) Baadhi ya wauza maziwa Tanzania hawazingatii kanuni za usafi kuanzia miili yao, mavazi, vyombo na mazingira kwa jumla ndiyo maanahusitishiwa mikataba yao ya kusambaza maziwa anapotokea mwingine anayejali usafi.Wateja wengine hulazimika kuyachemsha maziwa usiku kucha kabla ya kuyatumia kwa kuhofia magonjwa.

(c) Utafiti juu ya chanzo cha bidhaa au malighafi

Kabla ya kuanza kutoa huduma au bidhaa kwa wateja ambao uliwafanyia utafiti fikria.

(i) Je chanzo cha malighafi ni halali?

(ii) Bei zake ni nzuri na uhakika?

(ii)i Je vipi sera ya serikali kuhusu bidhaa hiyo?

Maswali hayo na mengine kama utapata majibu mazuri katika utafiti wako bila shaka biashara yako itakuwa nzuri.

# SURA YA PILI

# MRADI WA KUTENGENEZA CHAKI

Utengenezaji wa chaki ni moja ya mradi wa siri sana ambao ni mgodi unaweza kukupatia faida kubwa sana na ukasahau shida zote ulizowahi kupata katika maisha yako.

Kutokana na mradi huu ambao unafanyika kwa gharama za chini sana kutojulikana na watu wengi hapa Tanzania imekuwa ni mradi mzuri sana kuliko biashara yoyote ile hapa Tanzania kwa sababu miradi mingi mikubwa inahitaji mtaji mkubwa sana.

Mradi wa kutengeneza chaki ni mradi ambao unaweza ukaufanya kwa kutumia mtaji mdogo sana hapa Tanzania kuliko biashara yoyote ile unayoifikiria kuifanya.

Hapa tunakupa taarifa na maarifa madogo unayoweza kuyatumia kutengeneza chaki hizi zinazotumika katika shule mbalimbali hapa Tanzania ili ufanye biashara hii kwa faida kubwa sana na uifanye kuwa mkombozi wa maisha yako kiuchumi na wale wanaokuzunguka.

Katika kitabu hiki utafundishwa mambo mengi yatakayokusadia wewe unayetaka kuanza mradi huu, utafundishwa kwa njia rahisi sana zitakazo kufanya uweze kufanya mradi wako huu bila wasiwasi kabisa.

Utengenezaji huu wa chaki hauhitaji ujuzi mkubwa wala hauhitaji uende shule ukapate degree juu ya biashara hii, kila mtu anaweza akafanya hii kazi hata kama hujawahi kukanyaga darasani hata siku moja. Mradi huu unaweza ukafanyika sehemu yoyote ile hata vijijini kwa sababu hauhitaji umeme wala ujenzi wa kiwanda, ni wewe tu kuwa na nafasi nyumbani kwako, na kitu kikubwa ni kwamaba mradi huu hauna RISK, hii ni kwa sababu ni bidhaa isiyooza kama mlimaji wa nyanya. Ukilima nyanya uwezekano wa kupata hasara ni mkubwa sana kuliko mtu anayetengeneza chaki, mtaji unaoweza kuutumia kulima nyanya unaweza kuutumia kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza chaki nyumbani kwako.

Kitabu hiki kitakuelezea kiutalaamu jinsi ya kuanzisha kampuni ya utengenezaji wa chaki, na kama unatamani kujua na unatamani kumiliki kiwanda cha chaki kitabu hiki ni msaada mkubwa kwako.

**1.Kwanza, fanya utafiti wa soko.**

Biashara yoyote hapa Tanzania na hata nchi nyingine duniani, haiwezi kustawi kama hamna soko aya bidhaa hizo.

Inabidi uangalie kama kuna soko ambalo linaweza kukufanya uendelee kuwepo sokoni siku zote. Na kwa hapa Tanzania nakuhakikishia soko lipo la kutosha kwa sababu kuna shule nyingi sana na hasa uanzishwaji wa shule hizi za kata umefanya soko la chaki kuwa kubwa sana kwa sababu matumizi yake yameongezeka mara dufu, na makampuni yanayosupply bidhaa hii ni machache kuweza kuhudumia shule zote hapa Tanzania.

Wewe utakuwa shahidi, ni chaki za aina ngapi umeshawahi kuona sokoni, ni chache sana, sasa unaweza ukawa miongoni mwao na ukafanya vizuri sana. Katika kitabu hiki tutakufundisha jinsi ya kupata masoko na jinsi ya kuwafanya wateja wako waendelee kuwa wateja wako siku zote

## 2.Andika mpango mradi (business plan)

Hii ni hatua ya kwanza kabisa kufanya unapoanza biashara yako, kwa kuandaa mpango mradi wako utakufanya ujue malengo yako, soko lako, bajeti yako, soko lako na hata washindani wako wakoje n.k.

Mpango mradi wako unakupa wewe maono zaidi katika biashara yako ka kukufanya uweke juhudi zaidi katika biashara yako na hatimaye ufikie mafanikio yale uliyoyatarajia.

## 3.Chanzo cha mtaji (source of fund)

Hatua inayofuata ni kujua chanzo chako cha mtaji wa kuanzisha mradi huu wa chaki na kuuendesha vizuri. Kama huwezi kujitosheleza kipesa na unahitaji kufanya mradi huu basi usisite kuomba msaada katika taasisi za kifedha ili wakufadhili na utarudisha kwa sababu biashara hii ni ya uhakika. Pia unaweza kuangalia ni ndugu gani anaweza kukufadhili katika mradi huu na wakusaidie kuanzisha mradi huu.

Katika mradi huu utahitaji fedha kwa ajili ya kununua eneo la kufanyia kazi hii kama nyumbani kwako pamebana, pia utahitaji fedha kununua vifaa muhimu na malighafi za kutengenezea chaki hizo. Hata baada ya kuanza utahitaji pesa kuendesha biashara yako mpaka pale utakapoanza kupata faida.

Kumbuka kutangaza biashara yako ina gharama pia, lakini katika kitabu hiki tutakufundisha jinsi ya kutangaza biashara yako bila gharama kubwa kama ile ya kupeleka tangazo lako kwenye vyombo vya habari.

**4. Jitolee kufanya kazi katika kiwanda cha chaki bure.**

Kama wewe unaaza kufanya mradi huu, ni bora uanze kwa kujitolea bure kabisa kwenye viwanda vinavyotengeneza chaki hapa Tanzania ambapo viwanda hivyo si vingi sana, na kama vipo basi havizidi viwili au vitatu. Kuna kimoja kipo SIMIYU, unaweza ukaenda kuangalia wanafanya nini na hatimaye ukajifunza kwa ufanisi zaidi.

Lakini kitabu hiki kitakuelekeza jinsi ya kutengeneza chcki hizi bila hata ya kuhangaika kwenda kwenye viwanda vingine na ukafanya vizuri sana.

**5.Rasimisha biashara yako**

Kwa kuwa tayari una mpango mradi wako, sasa unaweza ukafanya utaratibu wa kurasimisha biashara yako ili iwe kisheria. Amua ni jina gani unataka kuiita biashara yako au mradi wako. Kwa mfano; P&B chalk production co, Quality chalk co, au NEEMA chalks. n.k

Muone mmwanasheria akusaidie ni jinsi gani ya kuandaa document za umiliki wa kampuni yako au mradi wako. Process hii inachukua kuanzia miezi miwili au chini ya hapo kama utafatilia kwa ukaribu zaidi.

**6.Tafuta eneo zuri**

Baada ya kufanya yote hayo, itakubidi utafute eneo zuri la kufanyia biashara hii, eneo zuri za kufanyia kazi hii ni sehemu za mjini ambako kuna urahisi wa kupata masoko na materials ya kutumia kutengenezea chaki hizo. Sehemu za mjini ndiko kuna shule nyingi zaidi kuliko vijijini na watumiaji wengine wa chaki kama mafundi nguo n.k lakini hata vijijini pia kuna shule nyingi sana hasahasa hapa Tanzania kuna shule nyingi sana za msingi na sekondari, kwa hiyo ni biashara nzuri pia kufanya vijijini na sio mijini tu.

**7. Andaa vifaa muhimu.**

Baada ya kufanya yote hayo hapo juu, cha unachotakiwa ni kuandaa vifaa muhimu vinavyohitajika katika kutengeneza chaki. Vifaa hivyo vinapatikana nje ya nchi na hata ndani ya nchi yetu hii ya Tanzania vinapatikana kwa wingi sana siku hizi. Vifaa hivyo vinaweza kupatikana katika maduka ya ujenzi, popote pale ulipo, wilayani na hata mikoani.

Vifaa hivyo ni kama;

- CHALK MOULD
- SCRAPERS
- PAINT BRUSHES
- DRYER
- HAND GLOVES
- PACKAGING MATERIALS kama branded cartons, and small boxes.

**8.Tafuta wasambazaji wa malighafi za chaki.**

Chaki ni malighafi ambayo inatengenezwa kwa malighafi rahisi sana na malighafi hizo zinapatikana kirahisi pia.

Malighafi hizo ni kama;

- PLASTER OF PARIS (P.O.P)

Hii ni malighafi muhimu sana, na ndio malighafi kubwa inayotakiwa kwa kiwango kikubwa sana katika utengenezaji wa chaki hizo tunazozizungumzia. Kitaalamu au kisayansi zinaitwa “Calcium carbonate”. Hii inatengeneza uji mzito na kukauka kwa haraka sana pale inapochanganywa na maji. Mbali na kutengeneza chaki, inatumika hospitalini kutengenezea muhogo(Kiswahili cha mtaani) kuzunguka mguu au mkono uliovunjika.

- MAFUTA YA KUPIKIA (mafuta ya kupikia)

Mafuta ya kupikia yanatumika kulainishia katika uzalishaji wa chaki. Mara nyingi hutumika kwa kuchanganya na mafuta ya taa ambayo huwa inatumika kulainishia matundu yanayopatikana kwenye mashine ya kutengenezea chaki (chalk moulds).

- RANGI (colour) – optional

Rangi hii kitaalamu inaitwa ultramarine blue ambayo itakupa rangi ya chaki unayohitaji.

- MAJI SAFI (clean water)

Maji yanatumika kuchanganyia malighafi ili kutengenezea chaki. Maji yanafanya plaster of paris kutengeneza uji mzito ambao utamwaga kwenye mashine ya kutengeneza chaki na uji ule kuganda mara moja kutengeneza stick za chaki ngumu.

**9.Mashine ya kutengeneza chaki.**

Mashine hii ni nyenzo rahisi sana ambayo imetengenezwa mahususi kwa ajili ya kutengeneza umbo sahihi la chaki. Katika mashine hiyo kuna matundu ambayo yanalingana na umbo la chaki ambapo uji uliotengenezwa kwa kuchanganya maji na plaster of paris (p.o.p) humwagwa na baada ya muda kidogo kutoa chaki zilizo ngumu na kwenda kuanika juani ili zikauke na hatimaye kufunga kwenye mabox na kupeleka sokoni.


# SCHOOL CHALK MACHINE

**PJ-CLAMP MOULD**

www.piusjustus.com

Whatsapp 0754745798/0659908078

**PRICE**
**Tsh.**
**300, 000/-**



**1NA MATUNDU 100**

**Pc 10, 000 za chaki kwa siku**

CM

PJ PROJECTS
Sulubisho La Mjasiriamali.
0659908078 | 0754745798

# SCHOOL CHALK MACHINE

**PJ- 200- CLAMP MOULD**

www.piusjustus.com

Whatsapp +255754745798/+255659908078

**PRICE**

**Tsh. 600, 000/-**





**It has 200 holes**

**Pc 20, 000 pcs per day**

CM

PJ PROJECTS
Sulubisho La Mjasiriamali.

**10. Ajiri wasaidizi sahihi.**

Kwa kuajiri wasaidizi sahihi na makini itakusaidia mradi wako wa uzalishaji wa chaki kwenda vizuri sana bila hata tatizo lolote. Inabidi utafute watu makini ili wasije wakakuharibia kazi yako ya uzalishaji, kumbuka inabidi utengeneze mfumo ambao watu wengi au wateja wako watakuamini na kupenda bidhaa yako, ukifanya ilimradi basi utapotea wateja wako na kampuni yako itakufa kabisa na hutaweza kuinuka kabisa, kwa sababu kurudisha imani ya watu itakugharimu sana.

**11.Tengeneza mfumo mzuri wa marketing.**

Mwisho unatakiwa utengeneze mfumo wa kutangaza biashara yako bila kutumia nguvu san alakini utengeneze wateja wa kudumu. Kwa sababu kuna ushindani, basi inabidi uwe mbunifu sana katika biashara yako; kwa mfano; kama mko watu wawili mnatengeneza bidhaa moja, jitahidi uwe tofauti hata kama mnatengeneza bidhaa inayofanana. Wewe katika katoni moja ya chaki zako, gharamia kuweka vitu vingine nadani ya katoni yako, unaweza kuweka kalamu za blue au nyekundu; hii itafanya shule nyingi kununua kwako kwa sababu kuna kitu cha ziada umeweka ambacho kinatumika na shule zao, walimu wataweza kutumia chaki hizo kufanyia vitu vingine kama kusahihishia n.k, sio chaki tu, unaweza kuchapisha kalenda ukaweka katika katoni zako, hii itwafanya wapende kununua bidhaa zako, na watakutangaza sana bila yaw ewe kutumia nguvu na hatimaye utaweza kuuza sana kuliko mshindani wako.

# MAKADILIO YA GHARAMA ZA UANZISHAJI NA FAIDA YA UTENGENEZAJI NA UUZAJI WA CHAKI.

- **Mashine inauzwa 300,000/-**

**Mashine hii ina matundu ya chaki 100**

**Kwa siku inaweza kuzalisha chaki 10,000 pcs sawa na carton 3-4**

- **Raw material**

**Plaster of paris (P.O.P)- mfuko wa kg 25 unauzwa 20,000/-**

| | | |
|---|---|---|
| **100 empty boxes @ 300/-** | = | **30,000/-** |
| **4 cartons (boxes) @ 2,500/-** | = | **10,000/-** |
| **1 litre ya cooking oil** | = | **2,200/-** |

..........................................................

**Tatal: 62,200/-**

**Note: Quantities**



- **1 kg of materials = 400 sticks of chalks.**
- **1 packet of chalk = 100 sticks of chalk.**
- **1 carton of chalk = 30 packets of chalk.**
- **1 packet of quality chalk mashuleni costs 3000 – 5000/-Rejareja mtaani 2500/-**
- **Jumla mtaani 1900/-**

## MAKADIRIO YA MAPATO KWA SIKU.

**Cost ya uuzalishaji kwa carton 4 = 62,200/-**
**Nguvu kazi (labour charge) = 10,000/-**
**Transport = 5,000/-**
**Total: = 77,200/=**



- **Mauzo mashuleni ambapo utakuwa unalipwa pesa kila mwisho wa mwezi kwani shule zinapata pesa kila mwezi;**

**Box moja linauzwa 3000/= x 30 (1catton) = 90,000/=**

**90,000/= x 4 cartons = 360,000/-**

**Ukitoa matumizi = 360,000 – 77,200 = 282,800/=**

**Kwa hiyo faida ya kuuzia mashule na ukawa unafata kwa mwezi, utatengeneza wastani wa Sh.**

**282,800/= ya faida kwa kila siku.**

**(kumbuka hiyo ni bei ya carton 4 tu za chaki)**

**ukiweza kuzalisha carton 100 na ukasambaza kwenye shule 100 kwa wastani wa carton moja kila shule utatengeneza wastani wa Sh.**

**282,800 x 14 = 3,959,200/- kwa mwezi mmoja tu.**

- **Tuzungumzie kipato utakachopata kwa kuuza reja reja.**

**Box 1 = 2500/= x 30 (1 caton) = 75,000/=**

**Kwa carton 4 = 75,000 x 4 = 300,000/=**

**Ukitoa matumizi = 300,000 – 77,200 = 222,800/=**

**Kwa kuuza reja reja kwa carton 4 utapata jumla ya Sh. 222,800/=**
**Kwa carton 100 utatengeneza 222,800 x 14 = 3,119,200/=**

- **Tuzungumzie kipato utakachopata kwa kuuza Jumla.**

**Box 1 = 1900/= x 30 (1 caton) = 57,000/=**

**Kwa carton 4 = 57,000 x 4 = 228,000/=**

**Ukitoa matumizi = 228,000 – 77,200 = 150,800/=**

**Kwa kuuza kwa Jumla kwa carton 4 utapata jumla ya Sh. 150,800/=**
**Kwa carton 100 utatengeneza 150,800 x 14 = 2,111,200/=**

**MUHIMU: kama wewe ni mfanya kazi;**

- **unapokuwa unaenda kazini, utaacha uzalishaji unaendelea nyumbani kwako, utakuwa huna hofu ya kuibiwa kwa sababu unajua ni chaki kiasi gani zinazotoka ndani ya kilo moja ya material.**
- **Material yote yanapatikana sehemu yoyote ulipo.**

- **Soko liko wazi. Unaweza kusambaza moja kwa moja mashuleni au kwa jumla kwenye maduka ya stationary**

- **Hakuna uwezekano wa kupoteza, kwani chaki ni bidhaa inayohitajika na shule kila siku.**

- **Mashine haihitaji marekebisho (service) unaweza ukatumia kwa miaka zaidi ya**
-

**HEBU JIULIZE;**

**Huu mradi hauwezi kukutajirisha kwa muda mfupi sana? Hauwezi kutatua matatizo yako wewe, mke wako, watoto wako, wazazi wako au hata jamii inayokuzunguka kwa kutoa misaada? Unaweza ukaajiri ndugu zako ambao wamemaliza vyuo hawana ajira, au hata wale ambao hawakupata bahati ya kusoma na wao wakapata ajira? Ni muda wa kufanya mradi huu ili uwaajiri ndugu zako ili wajitegemee kuliko kuwafanya wakutegemee kila siku.**

# JINSI YA KUTENGENEZA CHAKI NYUMBANI KWAKO

**Kwa kutumia mashine yenye matundu 100 unatakiwa kutumia robo kilo ya unga wa P.O.P (plaster of Paris) na kuchanganya na maji Robo Lita, hakikisha mchanganyiko wako sio mzito sana na usiwe mwepesi sana.**

**Baada ya kuchanganya mwaga ujimhuo juu ya mashine na kujaza matundu yote vizuri na uiache kwa muda wa dakika 8 hadi 10 kisha pakua chaki zitakuwa tayari kisha anika juani kwa muda wa siku moja hadi 2 chaki zitakuwa tayari kuwekwa kwenye vifungashio kwa ajili ya kupeleka sokoni.**

**Kwa kufanya hivyo utaweza kupata chaki zenye ubora wa hali ya juu.**

**Baada ya hapo nikutakie utekelezaji mwema wa madi huu.**


MUHIMU:

**Kwa mahitaji ya mashine unaweza kuwasiliana nami moja kwa moja kwa namba +255(0)754745798 au +255(0)659908078 ili niweze kukupatia mashine kwa bei nafuu sana.**

**Materials yanapatikana katika maduka ya ujenzi (ulizia PLASTER OF PARIS au P.O.P) na kama hawana ulizia Unga wa Gypsum wa kutengenezea mikanda ya gypsum bord za nyumba, hii inafaa pia kwani ina uwezo wa kuganda na kutengeneza chaki zenye ubora wa hali ya juu.**

**Packaging ya BOX utayapata katika viwanda vinavyotengeneza bidhaa hiyo. Kwa wale watakaohitaji box za kufungia bidhaa yako wasiliana nami nitakusaidia kupata box kwa bei nafuu kabisa na kukutumia popote ulipo Tanzania**

**ASANTE KWA KUNIAMINI.**
**Ni mimi mpenda maendeleo yako,**
**PIUS JUSTUS MULIRIYE**
**0754745798**
**0659908078**



# SURA YA TATU
# SABUNI YA MCHE (BAR SOAP)

**Sabuni hii ina historia ndefu. Imevumbuliwa kama miaka 500 iliyopita na wahindi na wachina. Africa ilifika kama miaka mia moja (100) iliyopita. Sabuni hii hutumika kwa kufulia na kuogea, kuoshea vyombo n.k**







Sabuni hii ina soko hapa Tanzania kwa 100% kwa sababu ni hitaji la kila siku katika jamii. Sabuni hii hutengenezwa kwa kutumia malighafi kuu nne;

- Mafuta
- Maji – yasiyo na chumvi
- Caustic soda
- Sodium silcate

KAZI YA CAUSTIC SODA NI:

- Kuyaunganisha mafuta na maji kuwa kitu kimoja
- Kuifanya sabuni igande
- Husababisha povu kutokea
- Kutoa uchafu kwenye nguo

# AINA YA MAFUTA YANAYOTUMIKA KUTENGENEZA SABUNI

Ni mafuta yale yenye tabia ya kuganda, kama vile mafuta ya mawese, mafuta ya nazi, mafuta ya nyonyo, mise au mbosa na mafuta ya wanyama.

Unaweza kupata sabuni iliyobora kama utatumia malighafi hizi kwa kipimo sahihi. Unashauriwa kuongeza kemikali nyingine inayoitwa sodium silcate (sio lazima) kwa ajili ya kuondoa muwasho wa caustic soda na kuleta umafuta kwenye sabuni yako na kuifanya iwe ngumu kuisha.

## FORMULA

| MAFUTA | CAUSTIC SODA | MAJI |
|---|---|---|
| Lita 1 | Gram 135 | Mills 350 |
| lita 3 | Gram 405 | Lita 1.5 |
| Lita 10 | Kg 1.35 | Lita 3.5 |
| Lita 20 | Kg 2.7 | Lita 7 |

## JINSI YA KUIANDAA (CAUSTIC SODA)

**Pima maji kwa kiwango unachotaka, weka ndani ya chombo cha plastic (ndoo), chukua caustic soda kwa kiwango ulichopima anza kuweka ndani ya maji kidogo kidogo huku ukikoroga kuelekea upande mmoja, koroga hadi vichanganyike utaona inatoa mvuke kisha acha ipoe kwa msaa 12 (epuka kugusa hayo maji kwa mikono) maji yatageuka na kuwa ya moto.**

## JINSI YA KUSAFISHA MAFUTA YA MAWESE

**Chukua mafuta bandika jikoni acha yachemke mpaka yatapoanza kutoa moshi. Chukua hydrogenPeroxide kwa kipimo kinachotakiwa, anza kuweka kidogokidogo kwenye mafuta utaona yanaanza kubadilika rangi na kuwa meupe kisha pima kwa kipande cha karatasi nyeupe utaona kama yametakata kisha epua yaache yapoe kiasi cha joto la maji ya kuoga.**

## ANGALIZO

**Zoezi hili ni hatari sana, unatakiwa kulifanya kwa uangalifu wa hali ya juu, ili kuepuka usumbufu huu, tunakushauri utumie mafuta masafi kama Mise, korie, olive oil, coconut oil n.k**

## JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI

**Chukua sodium sillgent mimina ndani ya caustic solution polepole huku ukikoroga mpaka vichanganyikane vizuri. Chukua mchanganyiko wa vitu vitatu, caustic solution anza kumimina kwenye ndoo ya mafuta polepole kama asali huku ukikoroga kwa haraka kuelekea upande mmoja mpaka uwe uji mzito. Mimina huo uji mzito kwenye mody au box acha ipoe kwa muda wa masaa 6-8 baada ya kukauka toa kwenye mody/box kata miche yako na gonga muhuri kwenye kila mche, fungasha sabuni zako kwenye mabox tayari kwenda sokoni.**

**Mfano wa Box za kugandishia sabuni (SOAP MOULD)**



# JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA MAGADI

Hizi ni aina za sabuni ya mche inayopendwa sana na watu wengi kwa sababu inatoa povu jingi sana na inatakatisha nguo na hata vyombo pia.

Sabuni hizi asili yake ni Kigoma, huko ndiko sabuni hizi hutengenezwa kwa wingi na husambazwa mikoa mingine pia, lakini katika kitabu hiki utajifunza jinsi ya kutengeza sabuni hizo.

MAHITAJI.

- Mafuta aina ya MISE/MBOSA lita 20
- Caustic Soda kilo 3
- Maji lita 10
- Rangi ya sabuni Vijiko 3
- Mwiko mkubwa wa kukorogea
- Ndoo kubwa (diaba)
- Box la kugandishia sabuni.
- Uzi wa kukatia miche ya sabuni




NB: Joto la caustic solution linatakiwa lisizidi 120-130 $^{\circ}$F, likizidi hapo sabuni itakuwa ngumu sana kupitiliza kawaida. Inashauliwa unapochanganya caustic soda na maji kuicha angalau masaa 1-3 kabla ya kutumika ili ipoe vizuri.
Kama caustic solution itakuwa baridi sana itafanya mafuta yawahi kuganda haraka sana na kufanya zoezi la kutengeneza sabuni kuwa gumu sana.

**JINSI YA KUTENGENEZA.**

1. **Chukua caustic Soda kilo tatu weka katika ndoo ya lita 10**
2. **Weka maji lita 10 kwenye ndoo yenye caustic soda**
3. **Koroga vizuri kwa umakini, maji yatageuka na kuwa ya moto, epuka kugusa kwa mikono yako, kisha funika na uiache kwa muda wa saa 24, ili ipoe vizuri.**
4. **Siku ya pili, weka mafuta yako katika ndoo kubwa/diaba, hakikisha mafuta yako yameyeyuka vizuri. Kasha chukua mchanganyiko wa Caustic soda na maji anza kumimina taratibu kwenye mafuta huku ukikoroga kuelekea upande mmoja, utaanza kuona mafuta yanaanza kuganda, endelea kukoroga mpaka utakapoona mafuta yamechanganyikana vizuri na maji yenye caustic soda.**
5. **Baada ya hapo mimina uji wako kwenye boksi kwa ajili ya kugandisha, funika box hilo kwa muda wa saa 24 mpaka 48 na sabuni yako itakuwa tayari.**
6. **Tumia uzi kwa ajili ya kukata sabuni yako**
7. **Ili kujua jinsi ya kutumia uzi kukata miche ya sabuni yako, tafadhari wasiliana nasi Whatsapp +255754745798 au +255659908078 tukutumie VIDEO inayoonyesha jinsi ya kukata kwa kutumia UZI.**




**Bonyeza**  **kuangalia video**



# SURA YA NNE.
# SABUNI YA MAJI (LIQUID SOAP)
# FOMULA NO. 1

**Sabuni hii iko hali ya kimiminika, ni tofauti na sabuni zingine.**
**Matumizi yake inafaa sana kufulia nguo, kuoshea vyombo, kupigia deki pamoja na kuoshea magari n.k.**

## MALIGHAFI ZAKE

- **Maji 20 lt**
- **Sles 1kg**
- **Sulphonic acid 1/2lt**
- **Industrial salt 1kg**
- **Cde vijiko 3 vya chakula**
- **Griceline Mills 50**
- **Perfume 25 mills (lemon)**
- **Rangi/colour blue Mills 5**

## FOMULA

| SLESS | SULPHONIC ACID | INDUSTRIAL SALT | CDE | GRICELINE | PERFUME | RANGI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kg 1 | Gm 500 | Kg 1 | Mills 50 | Mills 100 | Gm 5 | Mills 5 |
| Kg 2 | Kg 1 | Kg 2 | Mills 100 | Mills 200 | Gm 10 | Mills 10 |
| Kg 5 | Kg 2.5 | Kg 5 | Mills 250 | Mills 500 | Gm 25 | Mills 25 |

## JINSI YA KUTENGENEZA

1. Ndoo tupu
2. Chukua siles weka ndani ya ndoo 1kg
3. Chukua sulphonic acid weka ndani ya ndoo 500gm
4. Chukua chumvi weka ndani ya ndoo 1kg
5. Baada ya hapo weka huo mkorogo ndani ya ndoo.
6. Kisha changanya hizo malighafi ndani ya ndoo kwa kutumia
   mti au mwiko hadi iwe kama tope
7. Baada ya hapo weka maji lita 2 kisha anza kukoroga kuelekea
   upande mmoja.

8. Baada ya hapo endelea kukoroga huku ukiweka maji taratibu hadi zitimie lita 20, baada ya kutimia koroga kwa dk 10-15 kisha acha mpaka povu lipoe kabisa.

9. Baada ya povu kupoa weka griceline 50 mls, perfume 25 mls koroga kidogo kidogo.

10. Kisha weka rangi 5gm kama unapenda. Baada ya hapo sabuni yako itakuwa ipo tayari kwa matumizi au kuuzwa.

## SABUNI YA MAJI (MULT-PURPOSE)

## FOMULA NO. 2 (NZITO)

**Jinsi ya kutengeneza sabuni ya maji nzito LITA 6 inayotumika kwa kazi zote.**

## MALIGHAFI

**i. Nitrosol (thickner) – 240 gram**
**ii. Sulphonuic Acid – ½ lita**
**iii. SLS – vijiko 3 vya chakula**
**iv. Caustic Soda – kijiko 1 cha chakula**
**v. Soda Ash – kijiko 1.5 na nusu**
**vi. Form booster – vijiko vitatu vya chakula**
**vii. Maji safi – vikombe 5.5**
**viii. Perfume- kisi unachohitaji**
**ix. Rangi – kiasi unachohitaji**

# HATUA ZA UTENGENEZAJI

- Weka maji lita 3 kwenye chombo kasha yeyusha NITROSOL 240gram na ukoroge kwa muda wa nusu saa.
- Kwenye chombo tofauti weka SULPHONIC ACID ½ lita, SLES/TEXAPON 50mills, perfume kasha koroga kwa muda wa dakika 10, kasha weka maji lita 2.5 na ukoroge tena kwa dakika 10.
- Weka mchanganyiko namba 2 yaani (sulphonic, sless/texapon, na perfume) kwenye mchanganyiko namba 1.
- Weka Caustic soda iliyoyeyushwa kwenye maji na kukaa kwa masaa 24 iliyopoa.
- Weka SLS iliyoyeyushwa kwenye maji, kasha koroga pamoja.
- Weka Soda Ash iliyoyeyushwa kwenye maji na kukaa kwa saa 24, hii husaidia kupunguza ukali wa caustic soda.
- Weka Form Booster (hii huongeza povu) kisha koroga
- Weka rangi unayohitaji iliyoyeyushwa pembeni. (rangi ndogo sabuni huwa inapitisha mwanga (light), rangi nyingi (dark)) kasha koroga mchanganyiko huo

kwa muda wa dakika 10, kasha iache kwa muda wa saa 24 mpaka povu lote liishe, kisha weka katika vifungashio kwa ajili ya matumizi au kuuzwa.

# SURA YA TANO
# JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI YA MAJI YA KUOGEA
# (SHOWER JELLY)

**SHOWER JELLY, ni aina ya sabuni ya maji ambayo kazi yake kubwa ni kuogea. Sabuni hii ni mahususi kwa ngozi aina zote, na inapotumiwa huacha mwili ukiwa na harufu nzuri kabisa. Katika somo la leo utajifunza jinsi ya kutengeneza aina hii ya sabuni ukiwa nyumbani kwako na utapata matokeo mazuri kabisa.**
**Sabuni hii unaweza kufanya kwa ajili ya matumizi yako nyumbani au kwa ajili ya biashara.**

## KABLA YA KUANZA KUTENGENEZA KWANZA TUANGALIE TAHADHARI ZA KUCHUKUA.

- **Usigusanishe materials (chemicals) na ngozi au katika macho.**
- **Weka chemichals zote mbali na watoto.**
- **Usionje chemicals kwa ulimi wako.**

# ZIFUATAZO NI AINA ZA CHEMICALS ZITAKAZOTUMIKA KUTENGENEZEA SHOWER JELLY

- Nitrosol
- Sodium tripolyphosphate (STTP)
- Sodium bicarbonate
- Sodium Lauryl Sulphate (SLS)
- Chloroxylenol
- Tarpinol
- Glycol
- Vitamin E
- Colour
- Perfume
- Caustic soda
- Formaline or sodium Benzoate



## KIASI CHA MATERIALS CHA KUTENGENEZEA LITA 10 ZA SHOWER JELLY.

i. Nitrosol ..........................................................................60g
ii. Sodium tripolyphosphate .............................(STTP) 100g
iii. Sodium bicarbonate ....................................................100g
iv. Sodium Lauryl Sulphate .................................(SLS) 200g
v. Chloroxylenol ...........................................................25ml
vi. Tarpinol .....................................................................25ml
vii. Glycol ........................................................................25mil
viii. Vitamin E ................................................................50ml
ix. Colour .................................................................kijiko 1
x. Perfume ......................................................................40ml
xi. Caustic soda............................................................... 05g
xii.Formaline or sodium Benzoate.............................kijiko 1

## HATUA ZA KUTENGENEZA

- Weka kiasi cha maji kwenye ndoo
- Weka NITROSOL (60g) mpaka iyeyuke kwenye maji
- Yeyusha STTP (100g) kwenye maji (pembeni kwenye bakuli) kasha weka kwenye ndoo ya mchanganyiko, changanya vizuri.
- Yeyusha SODIUM BICARBONATE (100g) pembeni kasha changanya na mchanganyiko na koroga ichanganyikane vizuri.
- Yeyusha SLS (200g) pembeni kisha changanya kwenye mchanganyiko kwenye ndoo na changanya vizuri.
- Yeyusha CAUSTIC SODA (05g) kisha changanya kwenye mchanganyiko na koroga vizuri.
- Weka VITAMIN E (50ml) kwenye mchanganyiko
- Weka GLYCOL (25ml) kwenye mchanganyiko.
- Weka CHOROXYLENOL (25ml) kisha koroga.
- Weka TARPINOL (25ml) kisha koroga.
- Weka RANGI (tea spoon)

- **Weka PERFUME kisha koroga kwa muda vichanganyikane vizuri.**
- **Weka Preservative (FORMALINE or SODIUM BENZOATE)**
- **Baada ya hapo sabuni itakuwa tayari, weka kwenye VIFUNGASHIO.**

# SURA YA SITA

# SABUNI YA KUOSHEA VIGAE (TILES CLEANER)

**Tiles cleaner ni dawa ya kusafisha marumaru, masinki ya choo nay a kunawia. Hutengenezwa kwa kutumia malighafi zifuatazo.**

**i. Maji lita 20**

**ii. Hydrokloliki Acid Lita 1.5**

**iii. Sles gram 500**



## JINSI YA KUTENGENEZA

- **Pima maji Lita 20 weka kwenye diaba**
- **Weka siles Gram 500 anza kukoroga kuelekea upande mmoja**
- **Weka Hydrokololic Acid polepole koroga baada ya hapo itakuwa tayari weka kwenye vifungashio.**



## SURA YA SABA
## JINSI YA KUTENGENEZA DAWA YA KUSAFISHIA CHOO
## (DISFECTANTS)

**Disfectant ni dawa maalum ianyoua vijidudu vya magonjwa vinavyopatikana maeneo ya chooni, bafuni, kwenye karo, masinki na kwenye mifereji ya maji machafu. Dawa hii imebuniwa mahususi kwa kupambana na uchafu huo hivyo hata malighafi zake zimedhibitishwa ubora wa bidhaa yenyewe.**

**Dawa hii hutengenezwa na malighafi zifuatazo;**

**Maji 20lts, industrial salt 1kg, siles 1/2kg, sulphonic acid 250gm, formaline 100gm, perfume 25mls, colour 5gm**



## JINSI YA KUTENGENEZA

1. Maji lita 20
2. Weka siles 500gm ndani ya ndoo
3. Weka sulphonic acid 250gm ndani ya ndoo
4. Weka ndustrial salt 1kg ndani ya ndoo
5. Kisha koroga na mti hadi iwe tope
6. Kisha weka maji 2lt kwenye hiyo ndoo anza kukoroga kuelekea upande mmoja.
7. Baada ya hapo endelea kuweka maji kidogo kidogo mpaka yatakapotimia lita 20 huku ukiendelea kukoroga mpaka utakapojiiridhisha kama malighafi zote zimeyeyuka kisha acha mpaka baada ya masaa 7 ili povu lishuke.

8. Maada ya povu kushuka utatakiwa kumalizia malighafi zilizobakia. Formaline 100 mls, perfume 25 mls, colour 5gm

9. Kisha koroga kwa dk 5 baada ya hapo dawa yako itakuwa tayari kwa matumizi au kuuzwa.

# FORMULA

| MAJI | SLES | SULPHONIC ACID | CHU MVI | FOMALINE | RANGI | PERF UME |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lt20 | Gm 500 | Mils 250 | Kg 1 | Mills 100 | Gm 5 | Mills 25 |
| Lt40 | Kg 1 | Mills 500 | Kg 2 | Mills 200 | Gm 10 | Mills 50 |
| Lt60 | Kg 1.5 | Mills 750 | Kg 3 | Mills 300 | Gm 15 | Mills 125 |

# SURA YA NANE
# JINSI YA KUTENGENEZA HAND SANITIZER

Hand Sanitizer au VITAKASA MIKONO ni moja ya bidhaa muhimu sana ambayo hutumika kutakasa mikono na maeneo ambayo yanaweza kuwa yameathirika na vimelea vya bacteria.

Sanitizer hutumika hasa kusafisha mikono ili kujiweka safi na kujikinga na vimelea vya bacteria ambazo zinzweza kuwa hatari kwa afya yako.

Kuna aina kuu mbili za HAND SANITIZER ambazo ni LIQUID SANITIZER na GELLY SANITIZER.

Katika somo hili utajifunza jinsi ya kutengeneza aina zote za sanitizer zilizo bora kabisa.

## MALIGHAFI ZINAZOHITAJIKA

i. Alcohol
ii. Maji safi
iii. Hydrogen peroxide
iv. Glycerine
v. Carbormer
vi.P erfume – sio lazima



## JINSI YA KUTENGENEZA;

Mahitaji ya kutengeneza SANITIZER Mills 500 sawa na Nusu lita (1/2 ltr)

i. Alcohol – 400 Mills
ii. Maji safi – 75 Mills
iii. Hydrogen peroxide – 20 Mills
iv. Glycerine – 5 Mills
v. Carbormer – 2grams
vi. Perfume – matone manne (hii sio lazima)

## HATUA ZA UTENGENEZAJI (LIQUID SANITIZER)

- Weka alcohol kiasi cha Mills 400 kwenye chombo
- Huku ukikoroga weka maji safi kiasi cha Mills 75.
- Weka hydrogen peroxide Mills 20 huku ukiendelea kukoroga
- Weka ggryceline Mills 5 ukiendelea kukoroga.

Unaweza kuweka perfume wakati huu kama utahitaji lakini sio lazima

## HATUA ZA UTENGENEZAJI (GELL SANITIZER)

Pitia hatua zote za liquid sanitizer. Katika hatua ya mwisho huku ukikoroga weka CARBOMER kiasi cha Gram 2 huku ukiendelea kukoroga utaanza kuona mchanganyiko wako unakuwa mzito. Baada ya hapo weka kwenye vifungashio na uiche ikae masaa 72 kabla ya kutumika kama inavyoshauriwa na WHO, baada ya hapo itakuwa tayari kwa matumizi.

## SURA YA TISA
## SABUNI YA UNGA (DETERGENT POWDER)

Hii ni sabuni ya unga, hutumika kufulia nguo, inajulikana sana Tanzania kila mtu anapotaka kufua nguo hutumia sabuni hii.

Sabuni hii ina soko kubwa sana hapa Tanzania, inauzika kwa urahisi sana, watu wanaipenda sana, lakini sabuni hii haikutengenezwa ili itumike kufua nguo na mikono hii ni kutokana na kemikali zilizopo kwenye sabuni si-salama kufua nguo na mikono. Sabuni hii ya unga ilitengenezwa ili itumike kufua nguo na mashine.

### MALIGAHAFI ZAKE

1. Soda ash 6.5kg
2. STPP/sodium mentasiget 1.5kg
3. Sodium salphet 600gm
4. Nansa 10gm
5. Optical brightener 10gm
6. Sulphonic acid 1.3gm
7. Maji 400mils
8. Perfume 40mils



# MAELEZO KUHUSU MALIGHAFI

1. Muhimili wa sabuni ya unga huwa ni soda ash maana ndiyo iliyo nyingi kuliko malighafi zingine.

2. Pia ni muhimu kutambua kuwa ili uweze kutengeneza sabuni yeyote inayoitwa sabuni lazima huhusisha makundi mawili ya malighafi.

a)Uwe na malighafi ambayo inatoka kwenye kundi la Alikali
b) Pia uwe na malighafi inayotoka katika kundi la Asidi.

Mfano; Sodium Salphet hii inatoka kundi la Alkali, Ufacid inatoka kundi la Asidi, kwa hiyo ukizichanganya hizi malighafi yaani sodium salphet na ufacid utapata sabuni ya unga.

SWALI: Kama malighafi hizi mbili ndiyo zinaweza kuifanya iwe sabuni ya unga kwanini kuna mlolongo mrefu wa malighafi hadi zinafika 8?

- Tukianza kuangalia moja baada ya nyingine tutagundua kila moja imeingizwa hapo kwa makusudi maalum



Mfano;

- Soda ash ni kibebeo cha sabuni maana yake unaweza kutumia kibebeo kingine hata majivu, unga wa mahindi n.k.

- STTP/sodium mentasidget imeingizwa hapo ili kuongeza povu

- Nansa imeingizwa hapo ili kuzifanya hizi malighafi zichanganyikane.

- Optical brightener imeingizwa hapo ili kuleta mng'ao (kung'arisha)

- Maji yameingizwa hapo ili kuzifanya hizi malighafi zichanganyikane

- Perfume imeeingizwa hapo ili kuifanya hii sabuni iwe na marashi ili mtu anapofua nguo zake zinabaki na harufu nzuri ya manukato.

Vifaa vinavyotumika kutengeneza sabuni ya Unga:

1. Mabeseni makubwa au ndoo za plastic

2. Mwiko mkubwa au mpini kwa ajili ya kukorogea

3. Maski kama kifaa cha kujikinga ili usivute hewa chafu.

HATUA 5 za utengenezaji wa sabuni ya unga.

Ni muhimu kutambua kuwa hizi malighafi zimegawanyika makundi makuu mawili ambayo ni malighafi za unga-unga na malighafi za kimiminika.

a) Chukua malighafi na ungaunga zote weka kwenye beseni moja kisha koroga hadi zichanganyane hadi rangi ya optical brightener isionekane.

b) Chukua ndoo nyingine weka malighafi zote za za kimiminika kisha koroga hadi zichanganyikane na kuwa uji mzito hadi hapo utakuwa na mikorogo miwili tofauti ya unga-unga na ya kimiminika

c) Changanya mkorogo wa pili wa kimiminika na ule wa unga-unga viwe kitu kimoja kisha koroga hadi viwe kama unga wa mahindi uliomwagikiwa na maji.

d) Hatua ya nne ni kuanika kivulini, tumia turubai au mifuko ua sulphate baada ya masaa manne itakuwa imekauka na itakuwa tayari kwa kuuzwa.

e) Hatua ya tano ni kuiumua ili kuongeza faida. Ili kuumua utatumia detergent booster (hydrogen peroxide). sabuni ya unga unapoiumua. Mambo yafuatayo yanatokea;

i.Huongezeka mara mbili (2)
ii.Huwa nyepesi.
iii.Huchambuka na kuwa chengachenga.

SURA YA KUMI
UTENGENEZAJI WA BATIKI

## BATIKI NI NINI?

Ni nguo au kitambaa cha pamba kilichotiwa mshumaa na rangi kwa kuchora, kugonga, kuchovya, kunyunyiza.






VIFAA KWA AJILI YA KUTENGENEZA BATIKI:

1. Kitambaa cha pamba asilimia 100
2. Rangi za maji ya moto
3. Sodium hydrosulphate
4. Caustic soda
5. Sufuria ndogo
6. Ndoo za plastic
7. Mabeseni ya plastiki
8. Brush, sponji zilizochongwa
9. Vibao-vilivyochongwa
10. Kamba
11. Sindano
12. Mshumaa ghafi
13. Paraffin wax
14. Meza kubwa ya mita 3 kwa 1
15. Plastic conivas
16. Jiko la kuni au la mkaa

FORMULA

Kitambaa cheupe cha cotton mita 9

a) Maji ya moto lita 3
b) Sodium hydrosulphate vijiko 2 vya chakula
c) Caustic soda vijiko 2 vya chakula

Rangi ya batiki vijiko 3 vya chakula

## JINSI YA KUTENGENEZA

Andaa beseni kubwa na mwiko mkubwa kisha weka malighafi zote kulingana na kipimo ndani ya beseni weka maji ya moto lita 3 koroga kisha tumbukiza vitambaa ulivyo vifunga kwa dk 15.

(Kwa maelekezo zaidi jiunge na darasa letu kwenye GROUP YA WHATSAPP kwa kutuandikia ujumbe kupitia namba 0754745798 au 0659908078)

Ndani ya group utapata VIDEO za mafunzo kwa vitendo za jinsi ua kutengeneza BATIKI aina zote pamoja na masomo mengine kama vile SABUNI ZA MAGADI, SABUNI ZA MAJI, BATIKI AINA ZOTE, CHAKI, MISHUMAA, HAND SANITIZER, PERFUME n.k.)

Wasiliana nasi sasa WHATSAPP 0754745798/0659908078 tukuunganishe na darasa hilo.

# SURA YA KUMI NA MOJA
# MISHUMAA (CANDLE)

Mshumaa ni bidhaa inayoweza kutumiwa kupata mwanga majumbani, mahotelini na sehemu tofauti. katika dunia ya sasa hakuna mtu asiyejua bidhaa hii.

Bidhaa hii hutengenezwa na malighafi zifuatazo;

Paraffin wax, borie acid, stearic acid, stearing acid, utambi, hadna wax.

MAELEZO KUHUSU BIDHAA YA HIZI MALIGHAFI.

a) Stearic acid huufanya mshumaa ushikamane

b) Borie acid huufanya utambi uwake pasipo kutoa moshi

c) Hadna wax huufanya mshumaa uwe mgumu kuisha.

MALIGHAFI

1.Paraffin wax 2kg
2.Stearic acid vijiko 5 vya chakula
3.Borie acid vijiko 3 vya chakula
4.Hadna wax vijiko 4 vya chakula



NB: Unaweza kuweka rangi mshumaa wako ili uwe na muonekano wa kuvutia na kutokana pia na hitaji la soko. Utakuwa na muonekano wa pundamilia n.k.

JINSI YA KUTENGENEZA

Bandika sufuria jikoni ikipita moto kidogo, weka stearing vijiko 6 kisha weka hadna wax vijiko 4

Weka paraffin wax 2kg kwenye hiyo stearing pamoja na hdna wax acha mpaka iyeyuke na iwe maji. Chukua borie iweke kwenye chombo kingine halafu kata utambi uweke kwenye borie dk 3 baada ya hapo itoe na uanike dk 5.

Chukua huo mchanganyiko wa paraffin wax na uache upoe andaa maumbo uliyoandaa na weka utambi.

Anza kuweka huo mchanganyiko wako kwa awamu mbili tofauti ukianza kidogokidogo kwanza ili kuziba matundu. Baada ya hapo malizia kwa kujazia mody zako za mshumaa baada ya kujaza acha mpaka mshumaa upoe kabisa.

Ukishapoa ondoa kwenye mody na acha hadi ukomae vizuri tayari kwa kuuza.
NB: Kama mshumaa umeng'ang'ania kweenye mody tumbukiza kwenye maji ya moto.

# SURA YA KUMI NA MBILI
# HAIR SHAMPOO

Ni sabuni maalumu ambayo imebuniwa kwa ajili ya kusafisha nywele hata kama zimekaa muda mrefu bila kusafishwa. Hufanya nywele ziwe safi huondoa uchafu pamoja na kuua wadudu walioko kwenye nywele na huondoa mba kwenye nywele. Humfanya mtumiaji kufurahia matumizi yake.

MALIGHAFI

Shampoo hii hutengenezwa kwa kutumia malighafi zifuatazo;

Maji, siles, industrial salt, CDE, gryceline, perfume.

MAHITAJI

i. Maji 20lt
ii. Siles 1kg
iii. Industrial salt 1kg
iv. CDE 250 gm
v. Gryceline 50 gm
vi. Dye/colour 5gm
vii. Perfume 25ml



Weka kiasi cha maji ulichokiandaa kwenye diaba. Weka industrial salt anza kukoroga mpaka iyeyuke kabisa, weka CDE endelea kukoroga mpaka povu liwe jingi. Baada ya hapo weka siles andelea kukoroga dk 10 kwa nguvu mpaka iyeyuke. Acha mpaka siku ya pili au baada ya masaa 9 mpaka povu liwe limeshuka kabisa. Weka gryceline endelea kukoroga dk 3. Weka rangi au colour koroga kwa dk 3, baada ya hapo malizia na perfume koroga kwa dk 3.

Shampoo yako itakuwa tayari kwa matumizi au kuuzwa, weka kwenye kifungashio, bandika lebo, tayari kwa kupelekwa sokoni.



SURA YA KUMI NA TATU

# JINSIYAKUTENGENEZALOTION

Lotion ni aina ya mafuta ambayo yanatumika kulainisha ngozi hasa wale wenye ngozi kavu.

Lotion inatengenezwa kwa fomula mbalimbali ambayo unaweza kutengenezea nyumbani kwako.

Kwanza kabisa tutaanza na kutaja vifaa/materials yatakayotumika;




1. POLAWAX
2. CETYL ALCOHOL
3. PROPYLPARABEN
4. WHITE OIL
5. GRYCELINE
6. FRAGRANCE
7. MAJI

KAZI YA MALIGHAFI;

1.POLAWAX

Hii ni aina ya kemikali ambayo inasaidia kuweka uzito/thickness katika lotion. Hii inasaidia kuepuka kutumia malighafi nyingine nyigi ili kuleta uzito kwenye Lotion.

2.CETYL ALCOHOL

Hii ni kemikali ambayo ni ya lazima kutumia katika utengenezaji wa Lotion, kwa lugha nyingine inaitwa BINDING AGENT.

Inasaidia kuunganisha malighafi zilizoko ndani ya lotion. Mfano; huunganisha maji na mafuta yanapochanganywa pamoja.

3.PROPYLPARABEN

Hii ni kemikali inayotumika kama "Preservative" inayotumika kwenye vipodozi kuvitunza kwa muda mrefu.

4.WHITE OIL

Haya ni mafuta maalumu yanayotumika kutengenezea mafuta.

5.GRYCELINE

Hii hutumika kuleta unyevunyevu (moisturizing)

6.FRAGRANCE

Haya ni manukato ambayo yanakuwa na harufu mbalimbali za kila aina.

7.MAJI

Hii hutumika kuchanganya malighafi nyingine katika mafuta. (Is used as solvent)

JINSI YA KUTENGENEZA

Vipimo vinavyotakiwa;

Maji yaliyochemshwa na kupoa..............................66gm
Gryceline..............................................................03gm
Mafuta yaliyochemshwa.........................................15gm
Cetyl alcohol..........................................................3gm
Polawax...................................................................6gm
Propylparaben........................................................3gm

JINSI YA KUTENGENEZA;

1. Chukua chombo (sufuria) moja na weka Maji (66gm) pamoja na Gryceline (3gm) Kisha chemsha pamoja huku ukikoroga mpaka mchanganyiko huu upape moto wa kutosha kasha weka pembeni.

2. Hatua ya pili Chukua sufuria nyingine weka40White oil (15gm), Cetyl alcohol (3grm) na Polarwax (6gm), kasha chemsha pamoja mpaka viyeyuke pamoja, kisha weka pembeni.

3. Mchanganyiko huo katika vyombo viwili tofauti vichanganywe pamoja, yaani mchanganyiko mmoja weka ndani ya mwingine huku ukikoroga kwa muda wa dkk 5, utaona mchanganyiko wako unabadili rangi na kuwa CREAM, weka Propylparaben (3gm) koroga tena, wakati huu weka Perfume (fragrance) unayopenda.

4.Baada ya hapo acha upoe kabla kuwa mzito sana weka ndani ya kifungashio tayari kwa matumizi.

Kwa vipimo hivyo utapata 70Ml au ¼ Kikombe. Kama unataka kutengeneza kiwango kikubwa zidisha mara X unachokitaka.

Mfano; ukihitaji 700Mil utazidisha vipimo vyako mara 10. Tofauti na hapo zidisha kiwango unachotaka, x2, x3 au x4.

HAPO UTAKUWA UMEMALIZA KAZI YA KUTENGENEZA LOTION.

PJ PROJECTS
Suluhisho La Mjasiriamali.
0659908078 | 0754745798

# SURA YA KUMI NA NNE

## JAM (FRUIT)

Jam hutumika kwa kuliwa ikiwa imepakwa kwenye mkate na kumfanya mlaji afurahi kutumia jam mara kwa mara. Jam hutengenezwa na matunda kama maembe, papai, maparachichi, nanasi n.k.




## MAHITAJI

- Matunda 5kg
- Sukari 3kg
- Citric acid 2kg

## JINSI YA KUTENGENEZA

Andaa matunda kwa kuyasafirisha vizuri, yamenye na ondoa mbegu/kokwa kisha yakatekate vipande vidogovidogo na yasage kwa Brenda.

Kisha changanya sukari kiwango kinachotakiwa kisha kisha acha mchanganyo wako kwa muda wa dakika 30-40. Kisha ongeza citric acid uchanganye tena mpaka vyote viwe vimechanganyika sawasawa.

Bandika dufuria jikoni na kupika kwa joto la 100c-150c huku ukikoroga taratibu na utaona inazidi kuwa nzito.

Jinsi ya kukagua kama jam yako imeiva, chota kidogo na kijiko jaribu kumimina isipo miminika itakuwa ipo tayari, acha ipoe kidogo alafu weka vifungashio kisha peleka sokoni.



## SURA YA KUMI NA TANO

## UTENGENEZAJI MAFUTA YA MGANDO

Mafuta ya mgando hutumika kwa ajili ya kulainisha ngozi. Huwa yamegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo:

a) Mafuta ni mazito

b) Mafuta ambayo ni saizi ya kati

c) Mafuta mepesi.




MALIGHAFI

Paraffin wax 1/4kg, micro wax 1/2kg, white oil lita 2, Griceline 30mls, Perfume 12mls, Rangi ya wax 10gm (ukipenda)

JINSI YA KUTENGENEZA

- Tenga sufuria la maji jikoni, weka sufuria jingine kavu (tupu) juu yake

- Weka Micro wax ½ kilo, iache iyeyuke kabisa

- Baada ya hapo weka paraffin wax ¼ kilo

- Acha iyeyuke. Baada ya hapo weka white oil lita 2, kisha koroga polepole dk 15 kabla ya kuepuka.

- Griceline 30mils

- Weka perfume mils 12, kisha epua.

- Weka rangi 5gm kama ukipenda koroga dk 3
  Epuka weka kwenye vichupa tayari kwa matumizi.

NB: Mafuta haya yana viwango vya tbs, ni mazuri kwa ajili ya ngozi.

FORMULA YA MAFUTA SAIZI YA KATI
1.Macro wax kg1
2.White oil lita 1
Ukichanganya na kuyeyesha pamoja utapata mafuta saizi ya kati ambayo siyo mazito wala mepesi.

SURA YA KUMI NA SITA

# TAMBI ZA DENGU

Malighafi



- Unga wa dengu kilo 1
- Chumvi kijiko 1 cha chai
- Maji ½ lita
- Mafuta ya kula lita 1

JINSI YA KUTENGENEZA HATUA YA 1

Changanya chumvi kwenye maji robo lita kisha mwagia kwenye unga wako ambao umeuweka kwenye beseni huku ukichanganya na mkono taratibu, ongeza maji kidogo kidogo mpaka unga uchanganyike na kuwa kama ugali mabo sio mgumu sana wala sio laini sana.

## JINSI YA KUTENGENEZA HATUA YA 2

Kweka kalai lako jikoni kwenye moto wa wastani na mwagia mafuta kwenye kalia jaza unga wako kwenye mashine ya umbo la tambi kisha angalia mafuta yako yakisha chemka minya mashine ya tambi kuelekea kwenye kalaiutaona unga unatoka kwa umbo la tambi za jiko la stove ziache zidondokee kwenye kalai hadi ukiona kama zinatosha, zikate tambi mbichi zinazotoka kwenye mashine ili kutenganisha zilizomo kwenye kalai na mshine.

Hakikisha tambi zote zinazama kwenye mafuta na ukiona zinakua rangi ya kahawia zitoe kwa kutumia chombo kilichotobolewa ili kuvujisha mafuta mpaka hapo tambi zako zitakuwa tayari.



SURA YA KUMI NA SABA

# CLIPS

Clips hutengenezwa kwa viazi mviringo au ndizi na hutumika kama chakula cha ziada wakati wa safari na zina soko kubwa sana hapa Tanzania.

## MALIGHAFI



1.Viazi mviringo kg 1

2.Mafuta ya kula lita 1

3.Chumvi kijiko 1

4.Pilipili mbuzi 1

## JINSI YA KUTENGENEZA HATUA YA 1

Menya viazi na kuviosha kisha vikatekate kwa mtindo wa slesi, osha pilipili na kuitumbukiza kwenye maji ½ lita, koroga kwa kutumia kijiko ili kuyafanya maji yawe na pilipili kisha ondoa maganda na mbegu. Tumbukiza slesi kwenye maji ya pilipili kama unataka clips zako ziwe za pilipili halafu zianike juani ili kukausha maji.

JINSI YA KUTENGENEZA HATUA YA 2

Chemsha mafuta jikoni kwa kutumia kalai kisha kanga clips zako, kuwa mwangalifu kwa sababu hazichelewi kuiva na uivaji wake unategemea na moto hivyo ni kuanzia dk 3 na kuendelea, zikishaiva utaziepua zipoe na kuzifunga kwenye vifungashio vyenye lebo na kuzipeleka sokoni.



## SURA YA KUMI NA NANE

## WINDOW CLEANER

Dawa za kusafishia vioo vya aina zote mbalimbali kung'arisha na kupendeza.

Dawa hii inatumika kwa wakati unaposafisha vioo.




### MALIGHAFI

- Vinegar lt 1
- Sabuni ya maji lt 1
- Maji lt 10
- Rangi gm 5

### JINSI YA KUTENGENEZA

Bila kufuata mtiriliko wowote, changanya malighafi zote kwa pamoja na itakuwa tayari.

### MATUMIZI

Tumia kama ilivyo, kumbuka kuosha na maji masafi.

SURA YA KUMI NA TISA

# JINSI YA KUTENGENEZA DAWA YA KUONDOA MADOA (JIKI)

Hii ni moja ya dawa ambazo zinasaidia sana kuondoa madoa kwenye nguo ambayo imeshindikana kutakata kwa madoa ya UTOMVU, MCHUZI pamoja na uchafu mwingine sugu. MALIGHAFI ZAKE




1.Chloride Powder (britch)

2.Soda Ash

3.Maji.

JINSI YA KUTENGENEZA.

•Weka maji Lita 50

•Weka Chloride Powder Kilo 1

•Weka Soda Ash Kilo 1

Kisha koroga vyote kwa pamoja kwa dakika zisizopungua 20 kuelekea upande mmoja.

Baada ya hapo dawa yako (JIKI) itakuwa tayari kwa matumizi. Unaweza kuweka kwenye vifungashio na kupeleka sokoni. Unaweza kutafuta vijana wa kusambaza mtaani na ukatengeneza kipato kizuri.

Mauzo yake huwa ni kati ya Sh. 2000/- kwa lita moja, kwa lita 50 unaweza kutengeneza si chini ya Sh. 100,000/- kwa mtaji wa sh. 20,000/- tu.



SURA YA ISHIRINI

# UTENGENEZAJI UNGA WA LISHE

Unga wa lishe ni unga maalumu ambao unaleta nguvu na kuleta afya kwa watoto wadogo, wazee, wagonjwa, kwa kuwa hutengenezwa kwa malighafi zilizopo hapa hapa nchini na huuzwa kwa bei nafuu.

## MALIGHAFI




- Karanga 1.2kg
- Soya 1kg
- Ulezi 3kg
- Mahindi 3kg
- Mchele 1.5kg

## JINSI YA KUANDAA

Safisha ukezi, karanga, soya n.k. toa mchanga pamoja na vumbi. Kaanga soya kwenye moto hadi ibadilike na kuwa ya brown.

Saga kwa pamoja mchanganyiko huo halafu anika juani mpaka ikauke. Weka kwenye vifungashio peleka sokoni. Jihadhari kuwa msafi muda wote unapoandaa bidhaa za chakula.

(kaanga, toa maganda) saga kwa pamoja mchanganyiko huo halafu anika juani mpaka ikauke.
Weka kwenye vifungashio peleka sokoni.



# SURA YA ISHIRINI NA MOJA
# TOMATO SAUCE.

MALIGHAFI ZINAZO HITAJIKA

1.Nyanya Kg 1.5 ( Kilo moja na nusu )

2.Vitunguu Maji.Vitatu vilivyo menywa na kukatwa katwa vipande.

3. Mafuta ya Kupikia Vijiko Sita Vya chakula

4.Sukari Vijiko viwili vya chai.

5.Citric Acid.

6.Vinegar.Vijiko viwili vya chai.



## HATUA ZA KUFUATA WAKATI WA UTENGENEZAJI WA TOMATO SOUCE.

1.Saga mchanganyiko wa malighafi zote zilizo tajwa hapo juu kwa pamoja kwa kutumia mashine ya blender mpaka uwe rojorojo.

2.Tenga jiko la mkaa lenye moto wa wastani, kisha injika kikaangio kwenye moto halafu weka mafuta ya kupikia vijiko sita vya chakula.

3. Mafuta yakianza kuchemka, Anza kumimina mchanganyiko wako huo ndani ya kikaango hicho huku ukiwa una koroga upande mmoja mpaka umalize kuchanganya. Tumia dakika15 kufanya zoezi hili.

*Utakapo ona mchemsho wako umeanza kuwa uji uji, ipua na weka kwenye chombo safi tayari kwa matumizi.



# SURA YA ISHIRINI NA MBILI
# JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA TIBA

## 1. SABUNI YA MWAROBAINI/NEEM SOAP

Zifuatazo ni hatua za kutengeneza sabuni ya MWAROVAINI/NEEM SOAP.

- Andaa CAUSTIC SOLUTION
- Andaa Juice ya mwarobaini uliosagwa kwenye brender.
- Andaa mafuta (Mise, nazi, olive n.k)
- Andaa Mould/Umbo
- Andaa mwiko au Stick brender (Ya umeme)

### JINSI YA KUTENGENEZA

- Chukua juice ya mwarobaini weka ndani ya mafuta uliyoandaa na koroga kwa stick brender ili vichanganyikane vizuri.
- Chukua Caustic solution weka ndani ya mchanganyiko wa kwanza kisha koroga na stick brender mpaka upate uji mzito.
- Weka Perfume unayopenda.
- Mwaga mchanganyiko katika Umbo/MOULD na uiche kwa saa 24
- Kata vipande na uviache kwa muda wa saa 72 kabla ya kuanza kutumia. Hii hufanya kemikali zote kuchanganyikana vizuri na haziwezi kuleta madhara kwa mtumiaji.

VIPIMO VYA LITA 1 YA MAFUTA.

- Mafuta .........................................Lita 1
- Maji / Juice ya mwarobaini......Mills 1000/lita 1
- Caustic Soda ................................Gram 480
- Perfume ........................................Kiasi unachohitaji

MUHIMU: Ili kupata vipimo zaidi, zidisha vipimo hivyo mara kiasi unachohitaji.






# SURA YA ISHIRINI NA TATU
# JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA TIBA

## 2. SABUNI YA PARACHICHI/AVOCADO

Zifuatazo ni hatua za kutengeneza sabuni ya PARACHICHI/AVOCADO.

- Andaa CAUSTIC SOLUTION
- Andaa Juice ya parachichi iliyosagwa kwenye brender.
- Andaa mafuta (Mise, nazi, olive n.k)
- Andaa Mould/Umbo
- Andaa mwiko au Stick brender (Ya umeme)

### JINSI YA KUTENGENEZA

- Chukua juice ya parachichi weka ndani ya mafuta uliyoandaa na koroga kwa stick brender ili vichanganyikane vizuri.
- Chukua Caustic solution weka ndani ya mchanganyiko wa kwanza kisha koroga na stick brender mpaka upate uji mzito.
- Weka Perfume unayopenda.
- Mwaga mchanganyiko katika Umbo/MOULD na uiche kwa saa 24
- Kata vipande na uviache kwa muda wa saa 72 kabla ya kuanza kutumia. Hii hufanya kemikali zote kuchanganyikana vizuri na haziwezi kuleta madhara kwa mtumiaji.

VIPIMO VYA LITA 1 YA MAFUTA.

- Mafuta ..........................................Lita 1
- Maji / Juice ya Parachichi.........Mills 1000/lita 1
- Caustic Soda ................................Gram 480
- Perfume .......................................Kiasi unachohitaji

MUHIMU: Ili kupata vipimo zaidi, zidisha vipimo hivyo mara kiasi unachohitaji.



# SURA YA ISHIRINI NA NNE
# JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA TIBA

## 3. SABUNI YA CARROT

Zifuatazo ni hatua za kutengeneza sabuni ya Carrot

- Andaa CAUSTIC SOLUTION
- Andaa Juice ya Carrot iliyosagwa kwenye brender.
- Andaa mafuta (Mise, nazi, olive n.k)
- Andaa Mould/Umbo
- Andaa mwiko au Stick brender (Ya umeme)

## JINSI YA KUTENGENEZA

- Chukua juice ya Carrot weka ndani ya mafuta uliyoandaa na koroga kwa stick brender ili vichanganyikane vizuri.
- Chukua Caustic solution weka ndani ya mchanganyiko wa kwanza kisha koroga na stick brender mpaka upate uji mzito.
- Weka Perfume unayopenda.
- Mwaga mchanganyiko katika Umbo/MOULD na uiche kwa saa 24
- Kata vipande na uviache kwa muda wa saa 72 kabla ya kuanza kutumia. Hii hufanya kemikali zote kuchanganyikana vizuri na haziwezi kuleta madhara kwa mtumiaji.

# VIPIMO VYA LITA 1 YA MAFUTA.

- Mafuta ..........................................Lita 1
- Maji / Juice ya Carrot..................Mills 1000/lita 1
- Caustic Soda ................................Gram 480
- Perfume .......................................Kiasi unachohitaji

MUHIMU: Ili kupata vipimo zaidi, zidisha vipimo hivyo mara kiasi unachohitaji.



# SURA YA ISHIRINI NA TANO
# JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA TIBA

## 4. SABUNI YA PAPAI/PAPAYA SOAP

Zifuatazo ni hatua za kutengeneza sabuni ya Papai

- Andaa CAUSTIC SOLUTION
- Andaa Juice ya Papai iliyosagwa kwenye brender.
- Andaa mafuta (Mise, nazi, olive n.k)
- Andaa Mould/Umbo
- Andaa mwiko au Stick brender (Ya umeme)

### JINSI YA KUTENGENEZA

- Chukua juice ya Papai weka ndani ya mafuta uliyoandaa na koroga kwa stick brender ili vichanganyikane vizuri.
- Chukua Caustic solution weka ndani ya mchanganyiko wa kwanza kisha koroga na stick brender mpaka upate uji mzito.
- Weka Perfume unayopenda.
- Mwaga mchanganyiko katika Umbo/MOULD na uiche kwa saa 24
- Kata vipande na uviache kwa muda wa saa 72 kabla ya kuanza kutumia. Hii hufanya kemikali zote kuchanganyikana vizuri na haziwezi kuleta madhara kwa mtumiaji.

VIPIMO VYA LITA 1 YA MAFUTA.

- Mafuta ..........................................Lita 1
- Maji / Juice ya Papai..................Mills 1000/lita 1
- Caustic Soda .................................Gram 480
- Perfume ........................................Kiasi unachohitaji

MUHIMU: Ili kupata vipimo zaidi, zidisha vipimo hivyo mara kiasi unachohitaji.






# SURA YA ISHIRINI NA SITA
# JINSI YA KUTENGENEZA MAFUTA YA NAZI

Kuna aina kadhaa ya kutengeneza mafuta ya nazi, lakini kwa kawaida kuna aina kuu mbili (2) za kutengeneza mafuta haya. njia hizo ni;

1. Njia ya Kienyeji (jikoni kwako)
2. Njia ya kisasa (ya kutumia mashine-compressor)

## NJIA YA KIENYEJI:

Katika njia hii ya kienyeji, tumia hatua zifuatao;

Njia ya kwanza;

- Chukua nazi iliyokomaa
- Kuna nazi kwa kutumia njia yoyote uliyonayo kama una mbuzi, food processor, blender, grater n.k
- Weka katika chupa yenye mdomo mpana na uiweke itulie kwa saa 24. Au weka kwenye fridge.
- Toa mapovu ya juu. Toa mafuta ya katikati weka kwenye chupa nyingine ambayo ndio utayatumia. Maji yatakayobaki mwaga.

Njia ya Pili;

- Chukua nazi iliyokomaa
- Kuna nazi
- Chukua maji ya uvuguvugu halafu changanya na mikono yako kwa dakika moja hivi.

- lamua kwa kutumia chujio la nazi au cheese cloth. Unaweza kurudia mara kadhaa kuweka maji ya vuguvugu ili kutoa mafuta yote
- Ukishapata tui weka katika chupa na kuiweka masaa 24 ili mafuta yajitenge na maji. Au unaweza weka jikoni (medium heat) kwa muda wa saa moja au mpaka maji yameondoka na iliyobakia ni mafuta. Toa mapovu ya juu halafu weka mafuta yako katika chupa utakayotumia.

## NJIA YA KISASA (KWA KUTUMIA MASHINE)

Katika aina hii, mashine hutumika zaidi. Mashine inaitwa Compressor ambayo hufanya kazi ya kukamua mafuta hayo ya nazi.

Hatua za kufuata ni kama ifuatavyo;

- Kuna nazi zilizokomaa vizuri.
- Zikaushe juani, au kwa kutumia kifaa maalumu cha kukaushia (food drier)
- baada ya kukauka, mimina kwenye kinu cha mashine na washa mashine itaanza kukamua mafuta.




# Mashine ya Kukamua Mafuta ya Nazi na Nafaka aina zote





# SURA YA ISHIRINI NA SITA

## LEBO

Lebo ndio wasifu wa bidhaa. Lebo pia hubuniwa kwa mwonekano wake ikiwa na mambo yafuatayo;

1. Jina la bidhaa: buni jina zuri lenye mvuto ambalo mteja anavutiwa nalo na kulikumbuka kwa urahisi. Pia unaweza kutumia jina la kampuni yako, kikundi au jina lolote utakalobuni. Mfano; PIUS CLIPS, KIDOT CLIPS, DAD ACNE SOAP n.k

2. Utambulisho: andika utambulisho wa bidhaa ili mteja ajue ni bidhaa gani. Kwa mfano; Clips, Carrot Soap, Papaya Soap, Mwarobaini Soap n.k

3.Vilivyomo (ingradients): Andika vitu vyote ulivochanganya ili kupata bidhaa hiyo. Mfano mwarobaini, mafuta ya mawese, Caustic soda, chumvi na Glyceline.

4.Ujazo au uzito (quantity): andika ujazo au uzito wa bidhaa. Mfano 200mil, 25kg n.k

5.Tarehe au ujazo na idadi ya bidhaa ulizotengeneza (batch no) mfano 27-06-2012, 200g, 375

6. Tarehe iliyotengenezwa (mf. Date) na terehe ya mwisho wa matumizi (exp. Date)

mfano; Mfg: 27 juni 2016 Exp: 28 juni 2017

NB: bidhaa za sabuni na vipodozi hudumu kwa muda wa miaka mitatu na bidhaa za vyakula hudumu kwa muda wa mwaka mmoja.

Zipo lebo za aina mbili ya kwanza ni ile ya mhuri ambayo inagongwa kwenye bidhaa yenyewe na ya pili ni ile inayowekwa kwenye kifungashio ambayo ni ya karatasi yenye kung'aa (stika).



SURA YA ISHIRINI NA SITA

## VIFAA VYA USALAMA

Ni muhimu kujifunza kuhusu vifaa vya usalama ili uweze kujikinga kutokana na madhara yanayotokana na kemikali. Vifaa hivo ni kama ifuatavyo;

1.Ovaroli/Epilon

2.Miwani

3.Kofia ngumu

4.Gloves

5.Gambuti

6.Maski

7. Ndoo ya maji.



## SURA YA ISHIRINI NA NANE

## SEHEMU YA KUPATA MALIGHAFI

Malighafi hupatikana katika maduka maalumu na sio kila duka. Ukihitaji kufanya au kutengeneza bidhaa zinazokuhitaji kutumia kemikali inakubidi uende kwenye maduka wanayouza hizo malighafi. Ulizia maduka yoyote yanayouza vifaa vya kutengenezea batiki wanazo hizi malighafi kwa ajili ya wajasiriamali wadogo kama wewe

Zifuatazo ni namba za mawasilianao kwa baadhi ya maeneo;

1.Dar es salaam 0713 844 220
2.Dodoma 0682305459
3.Mwanza 0755420617
4.Arusha 0746425555
5.Njombe 0759106074
6.Shinyanga 0757860984
7.Musoma 0766183388



Kupata VIDEO za jinsi ya kutengeneza bidhaa mbalimbali wasiliana nasi WHATSAPP kwa namba 0754745798 au 0659908078

**BONYEZA HAPA KUJA WHATSAPP MOJA KWA MOJA**

# TAZAMA VIDEO 30 ZA MFUNZO KWA VITENDO HAPA

**Asante sana kwa kununua kitabu hiki, nasi tunakuzawadia Kozi ya VIDEO zaidi ya 30 zenye gharama ya Tsh. 450,000/- Bure kabisa. Endelea kujifunza kupitia kozi hii kwa manufaa yako na familia yako.**



## **Bonyeza Picha hapo juu kutazama video**

# KUHUSU MWANDISHI

Pius Justus Muliriye ni mjasiriamali, mwandishi, mhamasishaji na mnenaji ambae ameamua kufanya kazi hii ya kuhakikisha kua unapiga hatua katika kuinua kipato chako kila siku kupitia anachokiandika na kukinena. Karibu sana ukutane naye kwenye kitabu hiki cha Kwanza cha."Jinsi ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za ujasiriamali"

Ni imani yangu kuwa maisha yako hayatakuwa kama yalivyokua baada ya kusoma kitabu hiki.



PJ PROJECTS
Suluhisho La Mjasiriamali.
0659908078 | 0754745798

**BONYEZA HAPA KUJA WHATSAPP MOJA KWA MOJA**

# JIUNGE NA GROUP YETU YA WHATSAPP



**BONYEZA HAPA KUJIUNGA**

PJ PROJECTS
Suluhisho La Mjasiriamali.
0659908078 | 0754745798